SHIRIKA LA RELI TANZANIA

RELI NA MATUKIO GAZETI

Kila Mwezi



Machi 13, 2020

Gazeti la Reli | Toleo Namba 5 | Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

# MAKATIBU WAKUU WA WIZARA WATEMBELEA MRADI WA SGR DAR ES SALAAM - MOROGORO - DODOMA



*Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu wakuu wa wizara tofauti nchini wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Reli na Kampuni ya Yapi Merkezi katika mlango wa kutokea wa handaki namba mbili lililopo Kilosa mkoani Morogoro*

Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu wa wizara tofauti nchini pamoja na sekretarieti ya baraza la mawaziri wakiongozwa na muwakilishi wa Katibu Mkuu kiongozi Mhe. Prof. Sifuni Mchome watembelea mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kipande cha Kipande cha Dodoma - Morogoro tarehe 2 Machi 2020.

Lengo la ziara hiyo ya siku mbili iliyoanzia tarehe 2 - 3 ni kuona maendeleo ya mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR kuanzia Dodoma hadi Dar es Salaam kwa kipande cha Morogoro - Dodoma - Singida chenye urefu wa Kilometa 422 ambao umefikia zaidi ya 28% na Dar es Salaam – Morogoro umbali wa Kilometa 205 ambao umefikia zaidi ya 75%.

Ziara hiyo ilianza Mkoani Dodoma ambapo Makatibu wakiwa na mwenyeji wao Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa walitembelea katika maeneo mbalimbali ya Mradi ikiwemo kambi kubwa ya mradi wa SGR iliyopo Ihumwa Dodoma, mahahandaki 4 yanayojengwa Kilosa mkoani Morogoro, kiwanda cha uzalishaji wa Mataruma chenyen uweo wa kuzalisha mataruma 1100 kwa siku kilichopo eneo la Kilosa pamoja na kuona kazi za ujenzi wa tuta, madaraja, makalavati na uwekaji mataruma, reli na nguzo za umeme kwenye tuta la reli

Akiongea katika ziara hiyo Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano sekta ya uchukuzi Dkt. Leonard Chamuriho amesema kuwa Mkandarasi anapiga hatua katika ujenzi na usanifu wa njia ya Reli na kazi kubwa inafanyika usiku na mchana.

Ziara yetu hii ni ya siku mbili Machi 2 - 3, 2020, leo tumetembelea kipande cha Makutupora hadi Morogoro tumeona kazi kubwa inafanyika hasi katika ujenzi wa mahandaki manne, kesho tutatembelea kipande cha Dar es Salaam – Morogoro, kazi inakwenda vizuri na tunatarajia itakwisha kwa wakati" alisema Chamuriho Naye Mwenyeji wa Msafara Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa amesema kuwa "Sisi kama TRC tunashukuru, ujio huu wa makatibu wa serikali katika mradi huu ambao ni mtambuka unaogusa wizara zote kwahiyo ni ugeni muhimu sana kwa sababu utaturahisishia utekelezaji wa mradi huu kwa kuwa watendaji wa

>> Inaendelea Uk. 2

## MAKATIBU WAKUU WA WIZARA WATEMBELEA MRADI WA SGR DAR ES SALAAM - MOROGORO - DODOMA

Na Mwandishi wetu TRC >> Inatoka Uk. 1

wizara tayari watakuwa na uelewa juu ya changamoto na fursa zilizopo katika mradi, hawa ni watu ambao tunafanya nao kazi moja kwa moja"

Aidha Kadogosa amewahakikishia watanzania kuwa mradi wa SGR unaendelea vizuri na utakamilika, "Nawahakikishia watanzania kuwa mradi huu kipande cha Dar es Salaam – Morogoro kuwa tumebakisha 25%, hivyo mwaka huu treni lazima itapita na watanzania watapanda kwa mara ya kwanza, tunaendelea vizuri na tuna uhakika 100%" aliongeza Kadogosa

Katibu Mkuu wa Viwanda na Biashara Prof. Riziki Shemdoe amesema kuwa Kitu ambacho amekiona katika mradi wa SGR angetamani kila mtanzania aje aone, kwa kuwa kazi iliyofanyika ni kubwa sana amemshukuru Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa maamuzi magumu aliyochukua, ujenzi huu umewanufaisha sana wawekezaji wadogo wadogo, wakulima na wafugaji wakati wa ujenzi na pindi utakapokamilika.

Makatibu hao wameonesha kufurahishwa na maendeleo ya mradi huo na namna ambavyo umesanifiwa kwa kuzingatia mazingira ya kitanzani pamoja na namna ambavyo wananchi wameshirikishwa moja kwa moja katika usanifu na ujenzi wa miundombinu ya reli hiyo ikiwemo vivuko vya magari, wanyama na watembea kwa miguu. Mradi huu utakapokamilika unatarajiwa kuleta manufaa kwa Shirika na uchumi wa taifa kwa ujumla kupitia usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo.

## TRC YAZINDUA GAZETI

Gazeti hilo limezinduliwa likiwa na lengo la kuelimisha umma na kutoa taarifa kuhusu huduma zinazotolewa pamoja na miradi ya kimkakati inayosimamiwa na kuratibiwa na Shirika ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa – SGR, uboreshaji na ufufuaji wa reli ya kati – TIRP na ukarabati wa mabehewa.

Kwa upande mwingine gazeti litatoa fursa kwa wadau mbalimbbali yakiwemo mashirika, kampuni na taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi kutumia gazeti la reli kutangaza biashara na huduma wanazotoa kwa lengo la kutoa taarifa kwa jamii.

Gazeti lilikua likitoka kwa njia ya mtandao mara moja kwa mwezi kuelezea shughuli na matukio ambayo hutokea katika majukumu ya kila siku ya TRC na kuwekwa katika tovuti ya shirika (trc.co.tz) na kusambazwa kupitia mitandao ya kijamii.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi amelipongeza Shirika kwa kuandaa gazeti ambalo litakuwa na mchango mkubwa kwa Shirika na Serikali hasa katika kutoa taarifa kwa umma kuhusu miradi ambayo Serikali ya awamu ya tano inatekeleza kupitia Shirika la reli Tanzania.

Aidha, Prof. Kondoro amesisitiza kuwa wananchi wanayo haki ya kupata taarifa hivyo Gazeti hili limekuja muda muafaka ambapo Shirika liko katika mabadiliko chanya kiutendaji hivyo umma utapata fursa ya kufahamu mengi.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa, ametoa wito kwa mashirika, taasisi za Serikali na binafsi kutumia gazeti la shirika kutangaza biashara na huduma wanazotoa, hivyo itasaidia huduma na bidhaa zao kujulikana kwa kuwa gazeti hilo litapatikana mtandaoni na kwenye treni ambapo treni hubeba watu wengi, hivyo taarifa zao zitawafikia watu wengi kwa urahisi.

## WANAWAKE TRC WAADHIMISHA SIKU YA MWANAMKE DUNIANI

Na Mwandishi wetu TRC



Wanawake Shirika la reli Tanzania – TRC washiriki maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya *'Leaders Club'* Kinondoni jijini Dar es Salaam Machi 08, 2020.

Maadhimisho hayo yamefanyika yakiwa na kauli mbiu isemayo **"Kizazi cha usawa cha maendeleo ya Tanzania ya sasa na baadaye"** ikidhamiria kuleta usawa kwa wanawake wote bila kujali nafasi zao kimaisha na kimaendeleo.

Maadhimisho ya wanawake Duniani hufanyika kila mwaka mwezi Machi na kufikia kilele chake tarehe 08 ya mwezi huo kwa dhumuni la kuwakomboa wanawake na kuleta usawa katika jamii.

Katika kuadhimisha siku hiyo Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa amewapongeza wanawake wote nchini na Duniani kwa mchango wao katika jamii lakini pia ameeleza kuwa mabadiliko yaliyopo ni matokeo ya jitihada za kuhakikisha nafasi ya mwanamke katika jamii inatambuliwa na kuthaminiwa "mabadiliko yanawafanya wakina mama kushiriki moja kwa moja kwenye uchumi wa taifa, sisi kama Shirika tunatambua mchango wa wanawake na nafasi yao, wamekuwa na mchango mkubwa katika kuhakikisha shirika linatimiza majukumu yake" aliongeza Kadogosa

# TANZANIA NA BENKI YA STANDARD CHARTERED ZASAINI MKOPO WA UJENZI WA RELI YA KISASA - SGR

Na Mwandishi wetu TRC




*Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Philip Mpango (Mb) (kushoto), na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Standard Chattered (Tanzania) Bw. Sanjay Rughani, wakionesha Hati za Mkataba wa makubaliano ya mkopo nafuu baada ya kuweka saini, katika ukumbi wa Benki kuu Dar es Salaam hivi karibuni Februari, 2020.*

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Fedha na Mipango yatiliana saini makubaliano ya Mkopo wa Shilingi Trilioni 3.3 za kitanzania kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa reli ya Kisasa – SGR Dar es salaam - Dodoma - Singida, katika ukumbi wa Benki Kuu jijini Dar es Salaam hivi karibuni Februari, 2020.

Mkataba huo ni kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kisasa ambapo wabia wapatao 17 ikiwemo Serikali ya Denmark na Sweden kutoka Ulaya wakishirikiana na Benki ya 'Standard Chartered' ambaye ni mratibu wa mkopo huo wametoa mkopo wenye masharti nafuu kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Reli ya Kisasa kuanzia Morogoro – Dodoma - Singida.

Kwa niaba ya Serikali Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Philip Mpango na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Standard Chartered, Bw. Sanjay Rughani wameweka saini katika makubaliano hayo ambayo kwa kiasi kikubwa yatasaidia kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huo uliofikia zaidi ya 28% kwa kipande cha Morogoro – Singida, Serikali ya Tanzania imesimamia mradi huo kwa fedha za ndani tangu kuanza kwake mwaka 2018.

Aidha Dkt. Mpango amesema kuwa "Mradi huu wa kujenga reli ya kisasa ni mradi ambao unakwenda kubadilisha maisha ya watanzania, hivi sasa tayari umewaajiri watanzania zaidi ya 14000, mradi huu unatumia baadhi ya malighafi na vifaa ambavyo vinazalishwa hapa nchini hususani saruji, mchanga lakini nguvu kazi ni vijana wetu".

Dkt. Mpango ameongeza kuwa deni la nchi yetu bado ni himilivu na ni lazima tukope kwa sababu reli hii tunawekeza kwa miaka 200 ijayo. Pia amesisitiza kuwa Serikali itasimamia fedha hizo kuhakikisha zinatumika kama ilivyopangwa.

"Mkopo huu tunachukua na tutaulipa miaka 20 kwa hiyo muda tunao, nawashukuru wabia hawa ambao wameunga mkono jitihada za Serikali ya Tanzania za kubadilisha uchumi wa nchi kwa kutupatia mkopo wa Shilingi Trilioni 3.3". alisema Dkt. Mpango

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Standard Chartered, Bw. Sanjay Rughani amesema kuwa zoezi la kuwekeana saini ya makubaliano ya mkopo kwa ajili ya mradi wa reli ya kisasa ni hatua kubwa hasa katika suala la uchumi na uwekezaji katika sekta tofauti ili kuleta maendeleo "Afrika ni kipaumbele kwa biashara yetu na wateja kwa ujumla, tunajivunia kutumia utaalamu na fedha kusaidia serikali ya Tanzania kwenye mradi wa SGR". alisema Bwana Sanjay.

# WAJUMBE WA BARAZA LA WAFANYAKAZI TRC WATEMBELEA MRADI WA SGR DAR – MORO

Na Mwandishi wetu TRC



*Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa akitoa taarifa ya utendaji wa shirika kwa wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi TRC mara baada ya kufungua Baraza hilo katika ukumbi wa Mikutano uliopo jengo la 'Fire and Safety' Bandari jijini Dar es Salaam Februari, 2020.*



*Baadhi ya wajumbe wa Baraza Kuu la Wafanyakazi TRC wakitazama hatua tofauti za uzalishaji Mataruma katika Kiwanda cha Uzalishaji Mataruma kilichopo Soga mkoani Pwani, Februari, 2020.*

Wajumbe wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania – TRC watembelea mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR kipande cha Dar es Salaam – Morogoro Februari 2020.

Wajumbe wamefanya ziara hiyo kwa lengo la kuona maendeleo ya ujenzi ya Reli ya Kisasa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro ambacho ujenzi wake umefika zaidi ya 78%, ikiwa ni utaratibu wa Baraza hilo kutembelea Miradi ya Shirika kuona utekelezaji wake pindi unapoisha mkutano wa Baraza la Wafanyakazi ambalo lilifanyika kuanzia Februari 15 – 16, 2020 katika ukumbi wa 'Fire and Safety' Bandari jijini Dar es Salaam.

Wajumbe walitembelea katika stesheni za reli ya kisasa, kuanzia stesheni ya Dar es salaam ambao ujenzi wake umefika 65%, stesheni ya Pugu 85% na stesheni ya Soga 90%, sambamba na ujenzi wa Stesheni pia wamepata fursa ya kuona kazi nyingine za ujenzi zikiwa mbioni kukamilika.



*Meneja Msaidizi Mradi wa SGR Dar - Morogoro Mhandisi Ayoub Mdachi (kulia) akiwaelezea wajumbe wa Baraza TRC kuhusu maendeleo ya ujenzi wa Stesheni ya Kisasa jijini Dar es Salaam Februari 17, 2020.*

Wakiwa katika ziara wajumbe waliweza kupata taarifa kamili kuhusu maendeleo ya mradi katika kambi ya SGR iliyopo Soga wilaya ya Kibaha mkoani Pwani na kuona kiwanda cha kutengeneza mataruma ya reli ya kisasa ambacho huzalisha mataruma 1500 kwa siku huku wataalamu wanaofanya shughuli hiyo wengi wao wakiwa ni wazawa.

Akiongea katika ziara hiyo Kaimu Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Wafanyakazi Shirika la Reli – TRC Ndugu Amina Lumuli kwa niaba ya Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi TRC ameushukuru uongozi, Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika na Serikali kwa jitihada zinazofanywa chini ya Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli kuhusu Mradi huu wa Reli ya Kisasa.

"Tumekuwa na ziara ya mafanikio, Baraza la Wafanyakazi ni wawakilishi wa wafanyakazi tulianza mkutano siku ya Jumamosi lengo kuu likiwa ni kupitisha bajeti ya mwaka 2020/2021 pamoja na kuangalia mustakabali mzima wa taasisi, leo tunahitimisha Baraza kwa kutembelea Mradi" alisema Amina

Kwa upande wake Mhandisi Mipango Ndugu Enice Eryilmaz kutoka Kampuni ya Ujenzi ya Yapi Merkezi ameisifu Tanzania kuwa ni nchi ambayo hajawahi kukutana nayo, ina watu wachapakazi, wenye maarifa na elimu ya kutosha kuweza kufanya kazi katika Miradi mikubwa ukilinganisha na nchi ambazo wamewahi kufanya kazi kwani huwalazimu kuleta wataalamu kutoka nje kwa ajili ya kuwasimamia wataalamu wazawa ambapo ni gharama zaidi. Enice ameongeza kuwa hawakutegemea kupata nguvu kazi ya wataalam wazawa kwa idadi kubwa kwa sababu nchi zingine hufanya asilimia 50 kwa 50 ila kwa Tanzania wamepata asilimia 53.3 ya wafanyakazi watanzania hivyo ni jambo la kujivunia kwa Tanzania.

Aidha Katibu wa Baraza la Wafanyakazi Ndugu Edwin Kalisa amesema Mradi huu ni wa Watanzania, wajumbe wa Baraza ni vizuri watembelee kwani ni mabalozi wa kusambaza habari kwa wafanyakazi wa Shirika zima kuhusu yanayoendelea kwenye mradi ni ngumu kuwaleta wafanyakazi wote kwa pamoja kuja kuona mradi hivyo Wajumbe wawe mabalozi wa kufikisha haya, kuweza kukamilisha mradi huu.

# TANZANIA, BURUNDI NA KONGO KUJENGA RELI YA KISASA PAMOJA

Na Mwandishi wetu TRC



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Tanzania Mhe. Mhandisi Isack Kamwelwe na Waziri wa Uchukuzi wa Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo Mhe. Didier Mazenga Mukanzu watembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR jijini Dar es Salaam, Januari 2020.

Lengo la ziara ya Mawaziri wa nchi hizo mbili ni kuhakikisha maagizo ya Marais wa nchi za Tanzania, Burundi na Kongo ya kujenga reli ya kisasa kuanzia Uvinza – Msongati hadi Kongo yanatekelezwa kikamilifu ili mizigo ya Kongo na Burundi inayoingia katika Bandari ya Dar es Salaam iweze kusafirishwa kwa haraka na kwa bei nafuu, lakini pia kurahisisha muingiliano wa kibiashara katika nchi hizo.

Katika kutekeleza maagizo hayo tayari Tanzania na Burundi imekamilisha upembuzi na usanifu wa reli ya kisasa kutoka Uvinza Tanzania hadi Msongati Burundi ambapo nchi hizo mbili ziliamua kuchanga fedha ili kumuajiri Mhandisi Muelekezi aweze kufanya kazi ya usanifu wa reli hiyo, lakini katika hatua nyingine nchi za Kongo na Burundi zimekubaliana kuchanga fedha ili ziweze kufanya upembuzi na usanifu wa reli kutoka Msongati hadi Kongo kabla ya taratibu za kutafuta mkandarasi wa ujenzi wa reli hiyo kuanza.

"Mkutano wa kwanza tulifanya Kigoma, mkutano wa pili tulifanya Bujumbura na mkutano wa tatu tutafanya Lubumbashi mwezi wa tatu mwishoni 2020, maendeleo yaliyofikiwa mpaka hivi sasa kwa upande wa reli ya kutoka Uvinza mpaka Msongati usanifu umekamilika na usanifu huo tulichanga fedha Tanzania na Rwanda, kwenye mkutano wa juzi Burundi na Kongo wamekubaliana kuchanga fedha ili wafanye usanifu kutoka Msongati – Uvira hadi Kongo" alisema Waziri Kamwelwe

Mradi huu utakuwa ni wa pamoja kati ya Tanzania, Burundi na Kongo kutoka Uvinza – Msongati – Kongo, malengo ya mradi huu ni kupunguza gharama za usafirishaji kati ya nchi hizi tatu, kutokana na hilo tayari Serikali ya Tanzania imejenga Bandari kavu ya Katosho mkoani Kigoma ili Mabehewa yanayofika Bandari ya Dar es Salaam yawe yanapakiwa na kwenda kushushwa Katosho Kigoma

Naye Waziri wa Uchukuzi Kongo amemshukuru Waziri Kamwelwe, ameongeza kuwa ameona Mradi wa reli ya kisasa ambao umemfurahisha sambamba na Bandari ya Dar es Salaam, Waziri Mukanzu amesema kuwa anaihakikishia Mamlaka ya Bandari kuwa mradi wa reli kati ya Tanzania, Burundi na Kongo utakapokamilika biashara itakua kwa sababu mizigo itaweza kupitia Ziwa Tanganyika na mingine itapita kwenye reli mpaka Kongo "Sisi mawaziri tunawakilisha nchi zetu na Marais wetu walivyokubaliana ya kwamba ni vizuri wajenge reli itakayounganisha nchi hizi tatu" alisema Waziri Mukanzu

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli nchini Ndugu Masanja Kungu Kadogosa ameshukuru ujio wa mawaziri hao kuona mradi wa reli ya kisasa na Bandari ambavyo kwa pamoja vinashirikiana katika kuhakikisha mzigo unasafirishwa kwa gharama nafuu na kupunguza bei za bidhaa kwa walaji

# TRC YAENDELEA NA KAMPENI YA UELEWA KUZUIA AJALI NA HUJUMA DHIDI YA MIUNDOMBINU YA RELI

Na Mwandishi wetu TRC



*Timu ya Mawasiliano kutoka Shirika la Reli Tanzania - TRC ikiwa katika ofisi za AZAM TV mara baada ya kufanya mahojiano katika kipindi cha Mornging Trumpet kuhusu Kuuia Ajali na Hujuma dhidi ya Miundombinu ya Reli*

Shirika la Reli Tanzania TRC laendelea na kampeni ya uelewa kuhusu usalama wa miundombinu ya reli, matumizi sahihi ya alama za njia ya reli na mfumo mpya wa kukusanya maoni, kupitia mikutano ya wananchi na vyombo vya habari, Januari, 2020.

Lengo la Kampeni hii ni kutoa uelewa kwa watumiaji wa miundombinu ya reli wakiwemo madereva, watembea kwa miguu na wananchi kwa ujumla katika maeneo ambayo miundombinu ya reli imepita ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya alama za usalama wa njia ya reli pamoja na kuboresha huduma zitolewazo na Shirika.

Kampeni hiyo ilizinduliwa rasmi na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Focus Makoye Sahani Januari 28, 2020 ikiwa ni muendelezo wa kampeni zinazofanywa na Shirika kila mwaka kutoa elimu yenye lengo la kupunguza na kuzuia ajali, uharibifu na hujuma katika miundombinu ya reli, ambapo wataalamu kutoka Ofisi ya Usalama wa Reli, Mambo ya Kijamii, Jeshi la Polisi Reli na Ofisi ya Habari na Uhusiano TRC hushiriki katika kampeni hizo.

Zoezi hilo la kutoa elimu ya uelewa kwa wananchi kupitia vyombo vya habari na matangazo ya moja kwa moja linaongozwa na Mhandisi Maizo Mugedzi ambaye ni Mkuu wa kitengo cha ulinzi na Usalama wa njia ya reli, na Bi. Jamilla Mbarouk Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano pamoja na mtaalamu wa Masuala ya Kijamii Bw. Leodgard Lazarus Otaru wakishirikiana na timu nzima ya habari na uhusiano kutoka shirika la reli Tanzania – TRC.

Timu hiyo mpaka sasa imefanya ziara katika vyombo vya habari kutoa elimu ya matumizi sahihi ya alama za usalama wa reli, ikiongozwa na kauli mbiu inayosema "TRC KUZUIA AJALI NA HUJUMA DHIDI YA MIUNDOMBINU YA RELI INAWEZEKANA".

Miongoni mwa vyombo vya habari ambavyo timu hiyo imevitembelea ni pamoja na Azam TV, Radio One, TBC FM na Times FM lakini pia Shirika liliendesha Kampeni hiyo ndani ya treni za mikoani na mjini.

# KIPANDE CHA RELI MOSHI - ARUSHA KUANZA KAZI RASMI HIVI KARIBUNI

Na Mwandishi wetu TRC



*Muonekano wa sehemu ya kipande cha reli kilichofanyiwa ukarabati kwa awamu ya kwanza eneo la Nambala USA River Mkoani Arusha, mapema Januari, 2020.*

Usafiri wa treni za abiria na mizigo katika reli ya Kaskazini kutoka Moshi hadi Arusha umbali wa Kilometa 86 unatarajiwa kuanza hivi karibuni mwezi Aprili 2020 baada ya ukarabati wake kukamilika kwa zaidi ya 90%.

Mradi huo wa ufufuaji wa reli ya Kaskazini kuanzia Korogwe – Tanga – Moshi – Arusha ulianza rasmi utekelezaji wake mwaka 2017 kwa lengo la kurejesha huduma za usafiri wa treni katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha ambapo hadi kufikia Julai 2019 huduma za usafiri wa treni zilirejea kati ya Tanga na Moshi ambapo treni za mizigo ilianza kutoa huduma kuelekea Moshi na baada kufuatiwa na treni za abiria.

Kazi kubwa iliyofanyika ya kubalisha reli ya zamani yenye uzito wa ratili 45 katika baadhi ya maeneo na kuweka reli yenye uzito wa ratili 60, kuboresha tuta, makalavati, madaraja makubwa na madogo na kuimarisha mifumo ya mawasiliano imekamilika kwa kiasi kikubwa na kuwezesha viberenge kuweza kufika hadi Arusha vikitokea Moshi mkoani Kilimanjaro

Meneja Mradi wa Ufufuaji reli Moshi - Arusha Mhandisi Shadrack Masawe, ameeleza jinsi kazi ya ufufuaji reli na ujenzi wa miundombinu wezeshi inavyoendelea "tunaondoa reli ya zamani yenye uzito wa ratili 45 na kuweka reli yenye uzito wa ratili 60 ili kuongeza mwendokasi na ufanisi katika ubebaji mizigo. Kipande hiki cha reli ya Moshi - Arusha kilikuwa kimeharibika sana, asilimia 85 ya tuta ilikuwa imechukuliwa na maji, madaraja mengi yalikuwa yamevunjika lakini pia ya reli 1300, mataruma 1400 na vifungashio 50,000 viliibiwa" alisema Mhandisi Masawe.

Aidha sambamba na ukarabati wa reli Shirika linaendele na uboreshaji wa miundombinu mingine ya reli ikiwemo sehemu za kushusha na kupakia mizigo, vilevile stesheni za Korogwe, Moshi, Lembeni na Arusha zinaendelea kukarabatiwa ili kuhakikisha abiria wanapata huduma ya uhakika pindi safari zitakapoanza.

Kurejeshwa kwa huduma ya usafiri kutaleta fursa za ajira na kukuza biashara kutokana na kuwepo kwa usafiri wa uhakika na nafuu kwa wafanyabiashara kusafiri na kusafirisha bidhaa zao



*Muonekano wa moja ya madaraja makubwa yaliyofanyiwa maboresho kati ya Moshi na Arusha hivi karibuni Januari 2020.*

# SHIRIKA LA RELI TANZANIA – TRC LAENDELEA NA ZOEZI LA ULIPAJI FIDIA MOROGORO NA DODOMA

Na Mwandishi wetu TRC

Shirika la Reli Tanzania – TRC limekamilisha zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi wa wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma ili kupisha ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR kipande cha pili kutoka Morogoro, Dodoma hadi Makutupora hivi karibuni Februari, 2020.

Fidia zinazolipwa ni fidia ya ardhi, nyumba, miti, mazao na maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya kuchimba vifusi na kumwaga ambapo Serikali kupitia Shirika la Reli hutoa fedha kwa walengwa kama fidia.

Maeneo mbalimbali ya Mpwapwa wananchi wamepatiwa hundi zao na asilimia kubwa ya wananchi hao wamekwishahamisha makazi yao na wengine wanaendelea na zoezi hilo la kuhamisha mali na makazi ili kupisha mradi.Wananchi wameupokea vema mradi huo wa kisasa unaondelea na kufurahishwa kwa kiasi kikubwa kwani imani yao ni mradi kuwaletea maendeleo mbalimbali ikiwemo ya usafiri pamoja na mzunguko wa biashara .



*Mhasibu kutoka Shirika la Reli Bi. Angelina Kibaja (wa tatu kulia) na Mtendaji wa kijiji cha Kimambila Bi. Beatrice Shayo (wa kwanza kulia) wakiendelea na zoezi la kugawa Hundi za fidia kwa wananchi wa kijiji cha Kimambila, Morogoro Mvomero mkoani Morogoro Februari 2020.*

Maeneo ambayo baadhi ya wananchi wanatakiwa kupisha mradi wa SGR wilayani Mpwapwa ni pamoja na kijiji cha Msagali, Mnase, Msamalo, Godegode, Igandu, Chimwaga, Kimagai, Kisisi na Gulwe.

Aidha zoezi hilo limeendelea mkoani Morogoro ambapo wananchi katika wilaya ya Kilosa na Mvomero katika vijiji vya Kimambila, Chanzulu, Mkwatani, Kasiki, Mwasa, Kondoa na Mkadage wamelipwa fidia zao ili kupisha ujenzi wa reli ya kisasa – SGR, taratibu zinawataka wananchi hao kuhama katika eneo ndani ya siku 14 mara baada ya kupokea hundi za malipo yao.

Zoezi hilo ambalo linaendeshwa na maafisa kutoka Shirika la Reli nchini wakishirikiana na watendaji na wenyeviti wa vijiji wa maeneo hayo ambapo viongozi wa maeneo husika wameipongeza Serikali ya awamu ya tano Shirika la Reli pamoja kwa kuwa na juhudi za kujenga miundombinu nchini hususani reli mpya ya kisasa na kutimiza lengo la ulipaji wa fidia kwa wakati.

Mmoja wa Wahasibu wa TRC Bi. Teresia Bwire amesema kuwa changamoto ni nyingi zilijitokeza katika utoaji wa hundi ila ni jambo la kushukuru hadi limekamilika na wananchi wamekua na uelewa mkubwa wa kupisha mradi kwa haraka ili ujenzi uweze kuendelea.

“Wananchi wengi wameshahamisha makazi yao pamoja na wale wenye maeneo kama mashamba, madampo, na makaburi wameshayaachia, kiukweli wameonyesha ushirikiano wa hali ya juu” alisema Bi. Teresia Bwire.

Naye Mtendaji kutoka kijiji cha Igandu John Mandela amewakilisha watendaji wa Wilaya ya Mpwapwa kwa kuishukuru sana Serikali ya awamu ya tano ikishirikiana na TRC kwa utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa SGR kwani ni mradi mkubwa sana ambao utaleta chachu ya maendeleo kwa wananchi katika maeneo yote ya nchi

## TRC YASHIRIKI MAONESHO YA 23 YA USAFIRISHAJI BARANI AFRIKA

**Na Mwandishi wetu TRC,**

Shirika la Reli Tanzania – TRC lashiriki Mkutano na Maonesho ya 23 ya usafirishaji barani Afrika katika Hoteli ya Hyatt Regency jijini Dar es Salaam Januari 15 - 16, 2020.

Maonesho na Mkutano hayo yamefanyika kwa lengo la kuwakutanisha wadau wa sekta ya usafirishaji kuonesha huduma na bidhaa zao pamoja na kujadili namna ya kuboresha sekta usafirishaji barani Afrika.

Aidha, maonesho hayo yamefunguliwa rasmi na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Mhandisi Isack Kamwelwe na kusema kuwa Serikali ya awamu ya tano inatekeleza Miradi mikubwa katika sekta ya uchukuzi ikiwemo miradi miwili ya reli ambayo ni ujenzi wa reli ya kisasa – SGR na uboreshaji wa reli ya kati - TIRP ambayo itasaidia kusafirisha mizigo kwa wingi na haraka zaidi Tanzania na nchi jirani za Uganda, Rwanda, Burundi na Congo.

Kampuni zipatazo 18 zinazojihusisha na usafiri wa ardhini na majini zimeshiriki maonesho hayo yanayofanyika kila mwaka ambapo mwaka huu yamefanyika nchini Tanzania

Miongoni mwa Mashirika yaliyoshiriki ni pamoja na Mamlaka ya Bandari Tanzania – TPA, Shirika la Wakala wa Usafiri Majini – TASAC, Mamlaka ya Usafiri Ardhini – LATRA, Mamlaka ya Bandari Kenya, Shirika la Reli Tanzania pamoja na kampuni nyingine zinazojishughulisha na usafirishaji barani Afrika.

Waziri Kamwelwe amewashukuru waandaaji wa maonesho hayo kwa kuamua kufanya mkutano huo nchini Tanzania, na kuongeza kuwa Tanzania inawakaribisha wawekezaji na wadau wengine wa sekta ya usafirishaji kuwekeza katika sekta ya uchukuzi

## TRC YAREJESHA SAFARI ZA TRENI BAADA YA MAFURIKO KUHARIBU MIUNDOMBINU YA RELI

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania – TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa ameruhusu treni ya kwanza ya mizigo kuashiria kurejea kwa huduma ya usafiri wa treni za abiria na mizigo kati ya Kilosa – Gulwe, hivi karibuni Februari 2020.

Tukio hilo limefanyika Kilosa mkoani Morogoro kufuatia kusitishwa kwa Huduma za usafiri wa treni za abiria na mizigo kwa takribani wiki mbili na nusu kutokana mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa kuharibu miundombinu ya reli.

Mafuriko hayo yamesababishwa na mvua zilizotajwa kunyesha kwa wingi katika Mikoa ya Iringa, Manyara, Singida na Dodoma na kupelekea kuongezeka kwa maji katika mto Mkondoa na kuisomba reli ikiwa ni pamoja na kuharibu tuta la reli, madaraja, makalavati na baadhi ya stesheni za jirani na mto huo.

Mapema mwezi Januari 2020 Shirika lilisitisha huduma za usafiri wa abiria na mizigo kwa reli ya kati kutokana na mvua zilizoendelea kunyesha na kupelekea kuharibu miundimbinu ya reli hasa katika maeneo ya Kilosa - Gulwe umbali wa kilomita 120, ikiwemo kuharibika kwa makalavati, reli, stesheni, na madaraja.

Shirika limefanya jitihada za kuhakikisha huduma inarejea haraka iwezekanavyo kwa kutuma kikosi kazi cha mafundi na wahandisi wa kutosha katika eneo hilo ambapo wataalamu hao walikuwa wakifanya kazi usiku na mchana kwa kushirikiana na wahandisi wa mkandarasi kampuni za CCECC inayoboresha reli ya kati pamoja na YAPI MERKEZI inayojenga reli ya kisasa, ambao wote kwa pamoja wameshirikiana kurejesha huduma ya usafiri kwa njia ya reli.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi Mkuu ametoa pongezi za dhati kwa wahandisi na wafanyakazi kwa ushirikiano ambao umepelekea kurejesha huduma kwa wakati, hata hivyo mkurugenzi ameweka bayana kuwa njia iliyofunguliwa ni ya muda kutokana na uharibifu kuwa mkubwa na baada ya hapo Shirika litajikita kuimarisha na kutengeneza njia ya kudumu ambayo itakuwa ni suluhisho la mafuriko yanayotokea na kuharibu miundombinu ya reli katika maeneo ya Kilosa.

Kwa upande wake Mhandisi Felician Hechei, Meneja Mradi uboreshaji wa reli ya kati Kilosa - Gulwe ameeleza namna kazi ya uboreshaji reli ilivyofanyika kwa kuzingatia ubora na uimara wa eneo kutokana na miundombinu ya reli kuharibika kwa kiasi kikubwa. Aidha, wahandisi walizingatia sehemu ambazo wanaweza kurudisha njia kwa wepesi ikiwemo kuangalia maeneo yenye uimara ambayo yaliwezekana kuweka tuta la reli upya, lakini pia maeneo yaliyoharibika kwa kina kirefu walihamisha reli na kuweka upande mwingine wenye uimara zaidi.




*Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa akipeperusha bendera kuruhusu treni ya kwanza ya mizigo kupita katika njia ya reli ya kati eneo la Kilosa mkoani Morogoro hivi karibuni Februari 2020.*

Na Mpiga Picha Wetu TRC

## PICHA ZIKIONESHA SHUGHULI ZINAZOENDELEA KATIKA MRADI WA SGR DAR ES SALAAM - MOROGORO



*Muonekano wa Jengo la Stesheni ya Dar es Salaam likiwa limeanza kuwekwa vioo, usanifu wa jengo hili ambalo ujenzi wake umefika 65 umeakisi madini ya Tanzanite ambayo yanapatikana Tanzania pekee.*



*Muonekano wa Jengo la Stesheni ya Soga likiwa liko mbio kukamilika, usanifu wa jengo hili ambalo ujenzi wake umefika zaidi ya 90%, umeakisi Vazi la Kiremba linalovaliwa na wanawake nchini Tanzania.*



*Muonekano wa Jengo la Stesheni ya Pugu likiwa liko mbio kukamilika, usanifu wa jengo hili ambalo ujenzi wake umefika zaidi ya 85%, umeakisi Vazi la Kiremba linalovaliwa na wanawake nchini Tanzania.*




*Muonekano wa Jengo la Stesheni ya Ngerengere likiwa liko mbio kukamilika, usanifu wa jengo hili umeakisi Vazi la Kiremba linalovaliwa na wanawake nchini Tanzania.*




*Muonekano wa Reli na Nguzo za umeme wa Reli ya Kisasa - SGR zitakazokuwa zinaipa nisha treni zikiwa tayari zimetandazwa nyaya za umeme eneo la Soga Kibaha mkoani Pwani.*



*Muonekano wa kituo cha umeme cha Mpiji kitakachokuwa kikipokea na kusambaza umeme kwenye nguzo ili kuziwezesha treni za kisasa za umeme kutembea katika reli ya kisasa. Reli ya Kisasa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro itakuwa na jumla ya vituo 4 vya kupokea na kusambaza umeme.*

Na Mpiga Picha Wetu TRC

## PICHA ZIKIONESHA SHUGHULI ZINAZOENDELEA KATIKA MRADI WA SGR MOROGORO - SINGIDA



*Kulia ni muonekano wa kipande cha reli ya kisasa - SGR ikiwa imewekwa nguzo za umeme eneo la Mkata wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro. Kushoto ni reli ya zamani (Meter Gauge Railway).*




*Picha ya juu ikionesha Kambi kubwa ya ujenzi wa reli ya kisasa kipande cha Morogoro - Makutupora Singida iliyopo eneo la Ihumwa mkoani Dodoma.*



*Picha ya juu ikionesha moja ya Daraja kubwa la reli ya kisasa linalojengwa eneo la Mkata mkoani Morogoro katika mradi wa SGR kipande cha Morogoro - Makutupora mkoani Singida.*



*Maandalizi ya kujenga ukuta yakiwa yamekamika katika sehemu ya Handaki kuongeza uimara wa handaki*



*Mafundi wakiendelea na kazi ya kuimarisha Handaki namba mbili litakalopitisha reli ya kisasa kipande cha Morogoro - Dodoma - Singida katika eneo la Kilosa. Wataalamu hufanya kazi kwa awamu usiku na mchana ili kuhakikisha kazi hiyo inakwisha kwa wakati uliopangwa.*




*Muonekano wa ndani wa Handaki namba 2 lenye urefu wa Kilometa 1.032 likiwa limewekewa ukuta ili kuongeza uimara wa Handaki hilo linalojengwa Kilosa mkoani Morogoro kipande cha Morogoro - Dodoma - Singida.*

Na Mpiga Picha Wetu TRC

## PICHA ZIKIONESHA SHUGHULI ZINAZOENDELEA KATIKA MRADI WA SGR DAR ES SALAAM - MOROGORO



*Muonekano wa Jengo la Stesheni ya Dar es Salaam likiwa limeanza kuwekwa vioo, usanifu wa jengo hili ambalo ujenzi wake umefika 65 umeakisi madini ya Tanzanite ambayo yanapatikana Tanzania pekee.*



*Muonekano wa Jengo la Stesheni ya Soga likiwa liko mbio kukamilika, usanifu wa jengo hili ambalo ujenzi wake umefika zaidi ya 90%, umeakisi Vazi la Kiremba linalovaliwa na wanawake nchini Tanzania.*



*Muonekano wa Jengo la Stesheni ya Pugu likiwa liko mbio kukamilika, usanifu wa jengo hili ambalo ujenzi wake umefika zaidi ya 85%, umeakisi Vazi la Kiremba linalovaliwa na wanawake nchini Tanzania.*




*Muonekano wa Jengo la Stesheni ya Ngerengere likiwa liko mbio kukamilika, usanifu wa jengo hili umeakisi Vazi la Kiremba linalovaliwa na wanawake nchini Tanzania.*



*Muonekano wa Reli na Nguzo za umeme wa Reli ya Kisasa - SGR zitakazokuwa zinapitisha treni zikiwa tayari zimetandazwa nyaya za umeme eneo la Soga Kibaha mkoani Pwani.*



*Muonekano wa kituo cha umeme cha Mpiji kitakachokuwa kikipokea na kusambaza umeme kwenye nguzo ili kuziwezesha treni za kisasa za umeme kutembea katika reli ya kisasa. Reli ya Kisasa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro itakuwa na jumla ya vituo 4 vya kupokea na kusambaza umeme.*

Na Mpiga Picha Wetu TRC

# Yanayojiri katika Kampeni ya Uelewa kuzuia Ajali na Hujuma Dhidi ya Miundombinu ya Reli




*Mkuu wa Kitengo cha Usalama wa Reli Mhandisi Maizo Mgedzi akifafanua matumizi sahihi ya Alama za Usalama katika njia ya reli katika Studio za Redio One jijini Dar es Salaam, hivi karibuni Januari 2020.*



*Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano TRC Bi. Jamila Mbarouk akielezea namna Shirika linavyofikisha elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya alama za usalama wa reli na ulinzi wa miundombinu ya reli, katika Studio za Times Radio Dar es Salaam hivi karibuni Januari 2020.*



*Mtaalamu wa Masuala ya Kijamii kutoka TRC akitambulisha mfumo wa kupokea maoni wakati wa mahojiano katika kipindi cha Morning Trumpet cha Azam TV jijini Dar es Salaam hivi karibuni Januari 2020.*






*Majadiliano yakiendelea kuhusu Udhibiti wa Ajali na Hujuma dhidi ya Miundombinu ya Reli kati ya Maafisa kutoka Shirika la Reli Tanzania na Watangazaji wa TBC FM katika Studio za TBC FM jijini Dar es Salaam hivi karibuni Januari 2020.*

Na Mpiga Picha Wetu TRC




*Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Philip Mpango (kushoto), na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Standard Chattered (Tanzania) Bw. Sanjay Rughani, wakitia saini makubaliano ya mkopo nafuu kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR, Morogoro hadi Makutupora, mkoani Singida, hafla iliyofanyika Jijini Dar es Salaam Februari13, 2020.*




*Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli nchini Ndugu Masanja Kungu Kadogosa akionesha nakala ya Gazeti la TRC wakati wa hafla fupi ya uzinduzi iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano ofisi ya makao makuu TRC jijini Dar es Salaam hivi karibuni Januari 2020.*




*Mwandishi wa Habari TRC Bw. Ben Mwanantala akikabidhi zawadi ya kalenda ya Shirika kwa abiria Bi. Jane Alex baada ya kujibu swali wakati wa kampeni ya uelewa kuhusu matumizi ya alama za usalama wa njia ya reli wakati wa safari kutoka Dar es Salaam kuelekea Moshi, mapema Januari 2020.*




*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Reli Tanzania - TRC Prof. John Kondoro akionesha nakala ya Gazeti la Reli na Matukio wakati wa hafla ya uzinduzi wa gazeti hilo katika Ofisi ya Makao Makuu ya TRC Dar es Salaam hivi karibuni Januari, 2020.*



*Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi TRC wakifuatilia mada kutoka kwa Mwenyekiti wa Baraza hilo ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa katika ukumbi wa Mikutano uliopo jengo la kitengo cha Zimamoto na Uokoaji cha Bandari jijini Dar es Salaam Februari 15, 2020.*



*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakai TRC wakiwa katika picha ya pamoja walipotembelea kambi ya ujenzi wa reli ya kisasa - SGR iliyopo Soga Kibaha kuona maendeleo ya Mradi wa SGR kipande cha Dar es Salaam - Morogoro, hivi karibuni Februari 2020.*

# Wajibu wa Mtanzania katika Ulinzi wa miundombinu ya reli

**Na Mwandishi wetu TRC**

Takribani miaka 25 iliyopita Shirika la Reli Tanzania – TRC lilisimamisha huduma ya treni za abiria na mizigo kwa kanda ya kaskazini kwa mikoa ya Kilimanjaro, Tanga na Arusha, Mapema Desemba 01, 2019 Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini - LATRA Mhandisi Dkt. John Ndunguru alizindua rasmi treni ya kwanza ya abiria kutoka Dar es Salaam kuelekea Moshi mkoani Kilimanjaro.

Licha ya mafanikio lukuki katika sekta ya reli nchini hasa kwa kurejesha usafiri wa reli katika mikoa ya kaskazini bado watanzania kwa umoja wetu tuna jukumu la kuthamini, kutunza na kulinda miundombinu ya reli kwa sababu Serikali imetumia fedha nyingi katika kuhakikisha inawaletea watanzania maendeleo kupitia sekta ya usafirishaji na uchukuzi.

Kutokana na ufufuaji wa njia hiyo ambao umekuwa ni usafiri pendwa kwa wanakaskazini hasa katika unafuu wa gharama za usafiri na usafirishaji sambamba na uokoaji wa muda umekuwa ni chachu ya maendeleo ya mikoa hiyo na viunga vyake ambao umepelekea kuinua uchumi wa Shirika kwa kusafirisha abiria zaidi ya 10,000 tangu safari zianze.

Hivyo ni nafasi tena kwa watanzania wote kuisimamia na kuitunza miundombinu ya reli ili iweze kunufaisha Taifa kiuchumi na faida ya vizazi vijavyo. kumbukwe kuwa hivi karibuni tarehe 28, Januari 2020 Shirika la Reli Tanzania Kwa kuthamini jitihada za Serikali katika sekta ya reli, lilizindua rasmi kampeni ya uelewa katika ukumbi wa mikutano ofisi ya makao makuu Dar es Salaam, ikiwa na kauli mbiu "TRC KUZUIA AJALI NA HUJUMA DHIDI YA MIUNDOMBINU YA RELI INAWEZEKANA".

Kampeni ya uelewa ilifanyika katika vyombo vya habari tofauti Nchini vikiwemo TBC FM, Radio One, Times FM na Azam TV pamoja na mikutano katika maeneo ambayo reli imepita lakini pia elimu ilitolewa ndani ya treni za abiria kutoka Dar es Salaam mpaka Mkoani Kilimanjaro sambamba treni za mjini Pugu na Ubungo.

Wataalam wa masuala ya usalama wa miundombinu ya reli TRC pamoja na timu ya habari uhusiano TRC kwa pamoja waliendesha kampeni ya uelewa ikiwa na lengo la kutoa elimu kuhusu usalama wa miundombinu ya reli, matumizi sahihi ya alama ya njia ya reli, ulinzi wa miundombinu ya reli sambamba na mfumo mpya wa ukusanyaji maoni kwa lengo la kuboresha huduma za Shirika.

Kampeni hii ni endelevu ambayo hufanyika kila mwaka ikiwalenga wananchi wanaotumia miundombinu ya reli hususani madereva wa vyombo vya moto, watembea kwa miguu na wananchi waishio katika maeneo ambayo miundombinu ya reli imepita kwa lengo la kuzuia madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya alama za usalama wa njia ya reli.

Msukumo mkubwa umekuwepo kwa Shirika la Reli nchini kujikita katika kutoa elimu ya ulinzi na salama wa miundombinu ya reli kutokana na changamoto mbalimbali ambazo zimejitokeza katika maeneo ambayo reli imepita baada ya kazi kubwa kukamilika ya kurejesha usafiri wa reli.

Kwa kiwango kikubwa Shughuli za kibinadamu kandokando ya reli zinachangia uharibifu wa miundombinu ya reli, Kilimo, Ufugaji, biashara na makazi hupelekea tuta kuwa dhaifu na ardhi iliyo pembeni ya reli kukosa uimara na punde mvua zinaponyesha kutoka kwa sana hubomoa tuta na kuisomba reli. Ni wito kwa wananchi waishio maeneo ambayo miundombinu ya reli imepita hasa kuacha kuendesha shughuli za kibinadamu ambazo zimekuwa zikichangia uharibifu wa miundombinu.

Vitendo vya hujuma dhidi ya miundombinu ya reli hasa katika kipindi ambapo safari za Dar es Salaam - Moshi zilipoanza viliripotiwa, baadhi ya vitendo hivyo ni pamoja na wizi wa reli, mataruma na kuweka vitu vizito kama vyuma vizito, mawe na kufungua vifungashio vya reli ambapo vitendo hivyo ni hatari kwani husababisha ajali, vifo na kuharibu miundombinu ya reli na huzorotesha uchumi wa nchi licha hivyo taifa litapoteza nguvu kazi ambayo ni hasara kubwa kwa maendeleo ya taifa.

Kundi lingine ambalo ni vyema likawa makini katika kuhakikisha miundombinu ya reli iko salama ni madereva wa vyombo vya moto na watembea kwa miguu ambao ni wajibu wao na kuzingatia alama za usalama wa reli punde wanapofika kwenye makutano ya barabara na reli. Hivyo kwa kipindi ambacho njia ya reli imepambamoto katika kutoa huduma watembea kwa miguu na madereva wa vyombo vya moto wanatakiwa kuzingatia alama za usalama wa reli ili kujiepusha na ajali.

Ni ukweli usio pingika kuwa hatuwezi kusisitiza maendeleo bila kuthamini miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi ambayo ndio njia ya msingi kwa taifa kuelekea uchumi wa kati, hilo limethibitishwa na nchi nyingi zilizoendelea Dunia jinsi miundombinu ya usafiri ilivyoongeza kasi katika maendeleo ya nchi kutokana na thamani iliyopewa, Sekta ya reli inahitaji kuhakikisha usalama miundombinu na wananchi dhidi ya ajali na uharibifu wa mali.

# Yanayofanywa na TRC kuimarisha Miundombinu ya reli

**Na Mwandishi wetu TRC**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Shirika la Reli Tanzania imefanya juhudi ya kuhakikisha miundombinu ya reli nchini inaimarika kwa lengo la kufanya usafiri wa reli kuwa bora zaidi na kuongeza pato la taifa kupitia usafiri wa reli nchini.

Pamoja na changamoto nyingi ambazo Shirika linapitia katika utoaji wa huduma, TRC imekua ikikabiliana nazo ili kuhakikisha safari za treni ya abiria na mizigo zinaendelea kutoa huduma katika maeneo mbalimbali ya ndani ya nchi.

Changamoto hizo ni pamoja na uharibifu wa reli ya kati hasa kipande cha Kilosa – Gulwe ambacho kimekuwa kikisombwa na mafuriko kutokana na mvua zinazonyesha katika maeneo tofauti nchini, sambamba na hilo mambo mengine ni pamoja na Shughuli za kibinadamu zinazofanywa kandokando ya reli na kuathiri moja kwa moja uimara wa njia ya reli kwani shughuli za Kilimo, Biashara na Ufugaji zinachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa miundombinu ya reli.

Reli ya Kaskazini kutoka Korogwe hadi Arusha nayo ilihujumiwa kwa kiasi kikubwa, wananchi ambao sio wazalendo waliiba Mataruma, Reli na Vifungashio, hii inatokana na ufinyu wa maarifa na uelewa wa baadhi ya watu wanaoshindwa kutambua zuri na baya.

Hakika upo ubaya wa kuhujumu miundombinu ya reli kwani kunaweza kuleta maafa kama ajali ambao zinaweza kusababisha majeruhi, vifo na hasara kubwa ya mali.

Uzuri wa kutunza miundombinu ya reli tunauona pale tunapoutumia, mfano mzuri ni kwa wananchi wa Kaskazini ambao kwa sasa wanafurahi matunda ya uwepo wa njia hiyo, lakini kama wananchi wasio wazalendo wangeamua kuihujumu reli yote basi wasingekuwepo watu wengi wanaojivunia kurejea kwa huduma za usafiri wa reli ingepaswa aidha kujenga reli mpya ambayo ingetumia gharama zaidi au kuacha kabisa ili kuepuka gharama hizo.

Licha ya maafa na changamoto hizo kutokea chini ya Uongozi imara wa Menejiment ya TRC ikiongozwa na Mkurugenzi Mkuu Masanja Kadogosa kila jitihada zinafanyika kuhakikisha huduma zinaendelea kuwepo.

Mradi wa reli ya kisasa unaendelea kwa kasi ambapo hadi sasa awamu ya kwanza ya mradi Dar es Salaam hadi Morogoro imefika zaidi ya asilimia 78 na pia kwa awamu ya pili ya kipande kuanzia Morogoro hadi Makutupora – Singida umefikia zaidi ya asilimia 28, sambamba na mradi huo mpya Serikali inaendelea na Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya Kati Dar es Salaam - Isaka.

Kama tujuavyo kuwa usafiri wa treni ni usafiri wa uhakika na usalama , katika usafirishaji wa mizigo ama abiria na ni usafiri unaoaminika duniani kote hasa kwa nchi zilizoendelea kwa kuepusha kutumia gharama kubwa pamoja na kutumia muda mwingi barabarani hasa usafiri wa mijini.

Serikali kwa kuliona hilo, Shirika la reli Tanzania – TRC pia limeweka juhudi kuhakikisha kuwa treni za katikati ya miji zinafanya kazi kwa kusafirisha abiria kutoka katika maeneo yao hadi kuwafikisha katikati ya mji, kwa sasa treni za mijini zinafanya safari zake kati ya Pugu, Ubungo na Katikati ya Jiji.

Haya yote ni jitihada zinzofanywa ili kuona namna ya kutatua changamoto ya usafiri wa mjini ambapo kwa Shirika imekuwa fursa kwani imesaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza pato la Shirika na kupunguza msongamano wa magari barabarani ili wananchi waweze kwenda na wakati, muda ni mali na ukuaji wa uchumi katika nchi.

Aidha, katika Uanzishwaji wa njia mpya TRC imekamilisha upembuzi na usanifu wa mtandao wa reli ya Kisasa - SGR; Mtwara - Mbamba Bay yenye urefu wa KM 1,000, Tanga – Arusha – Musoma yenye urefu wa KM 1,000, Tabora - Kigoma yenye urefu wa KM 411 na Kaliua – Mpanda – Karemi yenye urefu wa km.360, Uvinza – Msongati (Burundi) yenye urefu wa KM 240. Pia Shirika linaendelea na usanifu wa reli ya Isaka – Kigali km.371. Pia usanifu wa mtandao wa reli jiji la Dar Es Salaam umekamilika na kwa jiji la Dodoma unaendelea.

Ili kuhakikisha Shirika linakuwa na maeneo ya kutosha kuweza kujenga miundombinu mipya ya reli Shirika limeendelea na ulipaji wa fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa, fidia hizo ni pamoja na nyumba, mashamba, vifuta machozi kwa ajili ya makaburi, madampo, shule, nyumba za ibada na ardhi. Kupitia fidia hizo wananchi wamenufaika hasa vijijini kwa kupata kipato ambacho kimewaletea maendeleo katika vijiji ikiwemo ujenzi wa nyumba za kisasa, biashara ndogondogo na hata kuanzisha shughuli za kilimo cha kisasa na ufugaji.

Bila shaka Serikali ya awamu ya tano kupitia TRC inaendelea kufanya vema katika ukuzaji wa miundombinu ya reli na kuupa kipaumbelele ukarabati na ujenzi wa reli ya kisasa ambao utaleta manufaa makubwa Afrika ya Mashariki pamoja na Afrika nzima kwa kuwa na ongezeko la usafirishaji wa abiria pamonja na mabehewa ndani na nje ya nchi.

## JE, kufanya KAZI ni sawa na kufanya MAZOEZI?

Na Dkt. Apolinary John

Unaweza kufanya kazi na kuwa na kitambi na pia waweza kufanya mazoezi na bado ukabaki kuwa nacho. Tabia ya kufanya mambo nusunusu haitupi faida, Ili kuzalisha tabia nzuri tunahitaji kufanya kitu hicho kwa mfululizo wa siku 21. Tunawaza vizuri mara nyingi, na pengine tukathubutu kutenda na tukaishia njiani kwa sababu sio tu ya kukosa maana bali kushindwa kujua faida ya kuendeleza jambo hilo.

Zamani tulikuwa tukisema kula kila kitu ni sawa kwa watoto hasa vile vyenye sukari (pipi, juisi, soda, keki, biskuti n.k) tukijua havina madhara. Kumbe tumejikuta tunazalisha matatizo kwa watoto hao, ndio maana sasa tuna watoto ambao wana magonjwa kama kisukari, shinikizo la damu na shambulio la moyo. Tuwape elimu sahihi mapema ili wawe salama, sio kula kila kitu na sio lazima kumaliza chakula ulichoagiza, kula kiasi ni afya pia. Ni lazima kuichagua afya kwa njia ya kula, kunywa, kazi na mazoezi ya kila siku.

Kazi ni utendaji wa jambo fulani kwa kutumia nguvu ya akili au ya mwili ili kufikia lengo fulani ambalo mara nyingi kazi hulenga kuleta faida ya kiuchumi ili kuweza kumudu maisha ya kila siku. Bila kazi hakuna maisha na ndio maana vitabu vinaandika asiyefanya kazi na asile. Tunampongeza rais wetu Mh. Dk. John Joseph Pombe Magufuli kwa kuwa mkweli na muwazi kwa umma wa watanzania kwa kuwa mfano wa kuchapa kazi nyingi zenye manufaa ya sasa na baadae kwa taifa letu.

Kama hatuko vizuri ni bora kutokwenda kazini maana tunaweza kupoteza heshima tunayostahili kwa kutoa huduma mbovu au kinyume na utaratibu. Kwa kutoa huduma bora kwa mikono yako kunahitajika ukomavu wa akili na roho kwa ujumla. Kazi huleta kipato na kwa msingi huo ni wajibu wa kila mtu, pia mchango muhimu katika jamii inayostahili kuheshimiwa na kutunzwa na serikali hadi mtu binafsi.

Kama hatuko vizuri ni bora kutokwenda kazini maana tunaweza kupoteza heshima tunayostahili kwa kutoa huduma mbovu au kinyume na utaratibu. Kwa kutoa huduma bora kwa mikono yako kunahitajika ukomavu wa akili na roho kwa ujumla.

Tunampongeza Rais kwa kuendelea kuhimiza watanzania kuchapa kazi kwa bidii na hata ikibidi tuchape kazi usiku na mchana ili kujipatia kipato na kuleta maendeleo ili kufikia uchumi wa kati. TRC kwa sasa watu wengi wamejionea Huduma zitolewazo hasa kuboresha usafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Kilimanjaro, hii ni Zaidi ya Huduma, maana watu wanafurahia kwa kuwaondolea msiba au adha ya usafiri.

Pongezi nyingi sana ziende kwa uongozi na watumishi wa shirika la reli Tanzania - TRC kwa kurudisha amani na furaha iliyokuwa imepotea kwa muda mrefu, takribani zaidi ya miaka 25.

Tukisema mazoezi na kazi ni tofauti tuna maaana kwamba kila kimoja kina malengo yake. Kazi hulenga kuleta afya ya mifukoni au uchumi katika ngazi ya mtu mmoja, familia, jamii na taifa letu kwa ujumla wake.

Mazoezi hulenga kujenga afya ya mwili, tusichanganye mazoezi na michezo kwani michezo huweza kuwa kazi na kuwa sawa na ajira nyingine yoyote.

Mazoezi ni vitendo vinavyofanywa na mtu ili kuuweka mwili katika hali ya afya njema na kuwa tayari kwa ajili ya jambo maalumu au kumfanya kuendelea kuwa mtu mwenye afya bora.

Inafaa uanze mazoezi hayo ukiwa peke yako au na kundi lako na ikiwezekana uwe na mwalimu au hata miongozo kutoka matumizi mazuri ya mitandao na kumbi maalumu (gymnastic centres). Anza mazoezi taratibu huku ukiwa na malengo yako na ratiba ambayo umeipa kipaumbele, kiafya tunakubali kuwa mtu ambaye amefanya mazoezi ni pale anapokuwa ameanza mazoezi na kutoka jasho mfululizo kwa muda wa dakika thelathini.

Mazoezi ambayo hayaambatani na kutoka jasho ni mazoezi dhaifu, unashauriwa kufanya mazoezi kwa muda wa dakika sitini mpaka tisini ili uweze kuwa katika kiwango kizuri na kuona faida yake. Dhumuni la kufanya mazoezi ni kuhakikisha viungo vyote vinatumika au kuhusika kwa namna moja au nyingine. Hivyo katika kazi unaweza ukajikuta hata kama unatoka jasho ila usihusishe viungo vyote hivyo hayo sio mazoezi.

Kazi inalenga kujiletea uchumi mzuri lakini kama nilivyokwisha sema mazoezi yanalenga kujiletea afya bora, hatukatai kuwa wapo watu wanafanya mazoezi kama kazi yaani wale walimu wa michezo au mchezaji lakini mchezaji pindi anapoingia uwanjani huwa sawa na mfanyakazi mwingine. Pia zipo kazi ambazo huwezi kuzihusianisha na mazoezi hasa zile za ofisini tena zile za kukaa, kusimama au kutembea.

Mifano ya mazoezi ni pamoja na kutembea kwa miguu, kukimbia, Kucheza mpira wa miguu au mikono, Kukwea milima, Kuendesha baiskeli, Kuogelea, sarakasi, Kuruka kamba, Mazoezi ya mwili mzima ya machine za mtetemo.

Kwa kutambua umuhimu wa mazoezi katika kujenga na kuziimarisha afya etu tunashauriwa kufanya mazoezi kila asubuhi na jioni kwa kuanza kwa kunyoosha viungo na kuupasha joto na kuendelea na mazoezi kulingana na kusudi au lengo la siku hiyo.




SHIRIKA LA RELI TANZANIA
Mtaa wa Reli/Barabara ya Sokoine
S.L.P 76959
Dar es Salaam
TANZANIA
Barua pepe;  info@trc.co.tz
Tovuti; trc.co.tz
Simu ya Bure; 0800 110 042



Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
SHIRIKA LA RELI TANZANIA

| | |
|---|---|
| MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk |
| MHARIRI MSAIDIZI | Sami Omary |
| MTAYARISHAJI | Sami Omary |
| MAKALA | Aziza Charles |
| HABARI | Tracylinda Nganga |
| PICHA | Seleman Kadiko |
| KIBONZO | Hassan Said |


tzrailways  TRC Reli TV

Reli Yetu | Maendeleo Yetu | Taifa Letu #TRCMpya